

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJISAFI NA MAJITAKA KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA JIJINI KIGOMA (“KIGOMA WSSA”) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-008

Mnamo tarehe 1 Julai 2018, Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya jijini Kigoma (KigomaWSSA) la kutaka kuongeza bei ya huduma zake za majisafi na majitaka kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Jedwali namba 1 hadi 4 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Maji za Sasa na Zilizopendekezwa (Shilingi kwa mita moja ya ujazo)

CUSTOMER Category	BEI YA SASA (TZS)		BEI INAYOPENDEKEZWA					
	Mita za ujazo	2017/18	2018/19		2019/20		2020/21	
			% Change		% Change		% Change	
Majumabani	0 - 10	780	86%	1,450	3%	1,500	72%	2,574
	0 - 20	780	99%	1,550	3%	1,600	87%	2,998
	Above 20	780	103%	1,580	3%	1,630	103%	3,301
Taasisi		1,160	64%	1,900	3%	1,950	3%	2,000
Biashara		1,200	67%	2,000	3%	2,050	2%	2,100
Viwanda		1,200	67%	2,000	3%	2,050	2%	2,100
Magati		500	100%	1,000	5%	1,050	5%	1,100

Jedwali 2 : Tozo za Sasa na Zilizopendekezwa za Kurejeshwa Huduma ya Maji Baada ya Kusitishwa (Shilingi kwa Marejesho).

Kundi la wateja	Bei zilizopendekezwa				
	2018/19	2019/20		2020/21	
		Badiliko		Badiliko	
Majumbani	10,000	0%	10,000	0%	10,000
Taasisi	15,000	0%	15,000	0%	15,000
Biashara	15,000	0%	15,000	0%	15,000
Viwanda	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Kioski	-	0%	10,000	0%	10,000
Wateja wakubwa	-	0%	100,000	0%	100,000

Jedwali 3(a) : Ada za Sasa na Zilizopendekezwa za Maunganisho Mapya ya Majisafi (Shilingi kwa maunganisho mapya) kwa wateja wa majumbani

Umbali kutoka kwenye bomba kubwa	BEI YA SASA (TZS)	BEI INAYOPENDEKEZWA					
	2017/18	2018/19		2019/20		2020/21	
		% Change		% Change		% Change	
0-10	Asilimia 20 ya gharama za maunganisho		60,000	17	70,000	14%	80,000
10-20			70,000	14	80,000	13%	90,000
20-30			800,000	13	90,000	11%	100,000
30-40			90,000	11	100,000	10%	110,000
40-50			100,000	10	110,000	9%	12,000

Jedwali 3(b) : Ada za Sasa na Zilizopendekezwa za Maunganisho Mapya ya Majisafi (Shilingi kwa maunganisho mapya) kwa wateja wa Taasisi, biashara na viwanda

Umbali kutoka kwenye bomba kubwa	BEI YA SASA (TZS)	BEI INAYOPENDEKEZWA					
	2017/18	2018/19		2019/20		2020/21	
		% badiliko		% badiliko		% badiliko	
0-10	Asilimia 20 ya gharama za maunganisho		80,000	13%	90,000	11%	100,000
10-20			125,000	8%	135,000	7%	145,000
20-30			160,000	6%	170,000	6%	180,000
30-40			195,000	3%	200,000	5%	210,000
40-50			225,000	2%	230,000	2%	235,000

Jedwali 4: Ada za sasa na zilizopendekezwa kwa huduma za Majitaka (Shilingi)

Aina ya huduma	Bei ya sasa	% badiliko	Bei inayopendekezwa				
	2017/18		2018/19	% badiliko	2019/20	% badiliko	2020/21
<i>Kwa kutumia magari ya KUWASA (kunyonya na kumwaga kwenye mabwawa)</i>	NA		100,000	0%	100,000	0%	100,000
<i>Kwa kutumia magari ya binafsi kumwaga kwenye mabwawa ya KUWASA</i>	NA		20,000	0%	20,000	0%	20,000

Kutokana na wasilisho la Kigoma WSSA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo, tozo za kisheria, gharama za ukarabati na uwekezaji.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 29 Novemba, 2018**, katika Ukumbi wa **NSSF** uliopo Kigoma mjini kuanzia saa 4:00 asubuhi ili kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la Watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu ndani ya kipindi kabla ya tarehe **10 Disemba, 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Makao Makuu ya EWURA, **GHOROFA YA NNE, JENGO LA LAPF, BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au **OFISI YA EWURA KANDA YA ZIWA GHOROFA YA NNE, UPANDE WA MBELE WA JENGO LA PPF PLAZA, BARABARA YA KENYATTA, MWANZA**, au ofisi za Mamlaka ya Maji Kigoma zilizo Kigoma mjini.

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
6 Novemba 2018